Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Pili – Tarehe 14 Juni, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mbele yetu kwenye *Speaker's Galley* ya Spika kuna wageni. Kwanza tuna *IGP* Mwema, halafu tunao wageni wengine wa *NGO* inayoitwa *Hans Sedel Foundation* ambayo inasaidia kutoa elimu kwa wanawake na Wabunge wanawake na kutoa elimu ya shughuli ndogo ndogo kwa wanawake na wanayo hoteli ambayo inaendeshwa kule Arusha. Imefundisha watu wengi kwa ajili ya shughuli za hoteli. Nadhani itakabidhiwa Wizara ya Maliasili na Utalii hivi karibuni. Nao ni Meneja Mkuu, Dr. Peter Witlaf, tuna Mkuu wa Idara katika *Sub Sahara Africa* Bwana Claus Lithent, halafu tuna *Resident Director* bwana Claus Solfrank na mke wake. Tunawakaribisha. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 11

**Ujenzi wa Barabara Kupitia Mradi wa *TASAF***

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ni muhimu sana katika maendeleo ya watu na vitu kwa msingi wa mawasiliano na uchumi na kwa kuwa pamoja na mambo mengine *TASAF* ilitegemewa kusaidia ujenzi wa barabara mbili muhimu lakini mradi wa *TASAF* ulimalizika kabla ya kuzijenga:-

Je, sasa *TASAF II* itasaidia kujenga barabara ya Ngenge - Rutoro iliyokisiwa kugharimu shilingi milioni 473 na ile ya Kamachumu - Bulamula - Ndolage iliyokisiwa kugharimu shilingi milioni 76?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu utekelezaji wa *TASAF* awamu ya kwanza katika Wilaya ya Muleba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Muleba ni moja ya Wilaya 40 za Tanzania Bara zilizokuwa katika utekelezaji wa mradi wa *TASAF* awamu ya kwanza. Katika awamu hiyo jumla ya miradi 35 ilitekelezwa katika Wilaya hiyo. Kati ya miradi hiyo, miradi 30 ilikuwa ni ya huduma za jamii na miradi 5 ilikuwa ni ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya ujenzi ililenga kuzinusuru kaya zilizo maskini zaidi kwa kuwapatia ajira ya muda ili fedha watakazopata ziwasaidie katika kupata mahitaji yao ya muhimu. Kati ya miradi 5 ya ujenzi, miradi miwili ilihusu matengenezo ya barabara ya Katoke hadi Nyawaiga yenye urefu wa kilometa 5.5 na barabara ya Kagoma hadi Rwazi yenye urefu wa kilometa 2.8. Ujenzi wa barabara hizo uligharimu jumla ya shilingi 57,129,414/=.

Aidha, miradi miwili ilihusu hifadhi ya vyanzo vya maji katika vijiji vya Kishanda na Bugaguzi na mradi mmoja ulihusu ukarabati wa mradi wa maji wa Kamishango.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Katika awamu ya pili, mradi wa *TASAF* unalenga kusaidia makundi matatu katika jamii. Makundi hayo ni:-

(1) Jamii zenye upungufu au ukosefu wa huduma za jamii, kundi hili litapewa msaada ili kuinua hali ya kiwango cha huduma za jamii katika maeneo yao kama elimu, afya, maji, usafi wa mazingira na kadhalika.

(2) Makundi maalum ya watu katika jamii wanaoishi katika mazingira magumu, kundi hili litapewa msaada kuwawezesha kuanzisha miradi ya kuongeza kipato, miradi ya uzalishaji huduma za afya majumbani kwa wenye UKIMWI na magonjwa nyemelezi. Walengwa katika kundi hilo ni pamoja na watoto yatima watu wenye ulemavu, wazee, wajane, walioambukizwa virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI.

(3) Kaya zinazokabiliwa na uhaba wa chakula lakini zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi. Kundi hili litapewa msaada kwa kuwawezesha walengwa kupata ajira ya muda na hivyo kupata kipato cha kuweza kununua chakula na mahitaji mengine ya msingi. Baada ya kushiriki katika kazi za ujenzi, walengwa watapata ujuzi wa kutengeneza miundombinu kama vile barabara, masoko, mifumo ya umwagiliji maji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, makundi yote ya jamii yanatakiwa kuomba msaada kwa kujaza fomu maalum ya kusudio la kutekelezwa mradi. Mradi utapatikana baada ya kupitiwa na kupitishwa na vyombo mbalimbali vya Halmashauri kama ilivyoelekezwa

katika taratibu za utekelezaji. Hivyo basi mradi utakaopata fedha kutoka *TASAF* ni ule tu utakaotokana na ainisho la jamii husika katika ngazi ya Kijiji/Mtaa na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi iliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge itapata fedha kutoka *TASAF* kama tu itaainishwa na jamii husika. Tungependa ifahamike pia kuwa kiwango cha juu kabisa cha mchango wa *TASAF* katika utekelezaji wa miradi ni dola za Kimarekani 30,000 kwa mradi mmoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimmiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara hii ambayo tulitegemea kwamba ingepata kujengwa kipindi cha *TASAF I* haikuwezekana na kwa kuwa gharama ya mradi huo wa kwanza hasa Ngenge kwenda Lutoro ni gharama kubwa eneo ambalo tangu dunia imekuwapo hawajawahi kuwa na barabara wanahitaji huduma ya elimu, afya na mazingira.

(a) Je, huduma hizi zitawafikia vipi kama Serikali haikuweza kuwapelekea barabara? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa wananchi watakapojaza fomu maalum wataweza kukubaliwa kuingizwa katika mradi wa *TASAF II* je, kiasi hiki cha shilingi milioni 30 labda 32 kwa hela za Kitanzania ningelishauri pengine kama inaweza je wapewe ili walau waweze kuweka *pavement* kwanza ya barabara ili baadaye waweze kuomba Serikali Kuu iweze kusaidia kukamilisha barabara hiyo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba arudie swali la pili bahati mbaya kwenye kona hii hatusikii vizuri. Swali la pili tafadhali.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongea kwa sauti pia.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia maswali yote mawili, kwanza lile la kwanza naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kuhusu swali la kwanza ni kwamba Serikali iko tayari kujenga barabara hiyo kwa utaratibu mwingine maana *TASAF* ni moja ya utaratibu wa kusaidia maendeleo ya wananchi, upo utaratibu wa kupitia Halmashauri ya Wilaya kwa hiyo, huu nao unaweza ukatumika au kwa kutumia Wizara ya Miundombinu, kwa hiyo, hayo yote yanaweza yakatumika kujenga barabara hiyo.

Kuhusu suala la pili, sawa kama watajaza fomu kwa kufuata utaratibu uliowekwa basi wataweza kupata hizo dola 30,000/=. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa imebainika kwamba wakati wataalam wa *TASAF* wanazunguka katika Wilaya zetu au Majimbo yetu kuwahamasisha na kutoa semina kwa walengwa wanataja pesa zilizotolewa katika mradi huo katika kila Wilaya lakini taarifa tuliyopewa sisi katika

Bunge hili ni kwamba zile pesa ziko *interms of USD* lakini wao katika maeneo yetu wanazungumzia *Tanzanian Shillings* sasa Serikali iweke wazi zile pesa ni *USD* au ni *Tanzanian Shillings*, kama ni *USD* basi waelekezwe wataalam wetu kwamba wataje gharama zile za miradi kama *USD* na siyo *Tanzanian Shillings* kwa sababu kuna tofauti ya thamani kati ya dola na shilingi. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni salama zaidi fedha hizo zikawa katika *USD* kwa sababu *currency* hiyo ni *stable* zaidi na ina maana mradi huo ukianza *convention* ya *USD* wakati huo utapata fedha ya Tanzania kwa wakati huo ya thamani hiyo itakayokuwepo, mathalani kama leo dola ni shilingi 1,250 na wakati mradi utakapotolewa dola itakuwa labda imeshakuwa 1,300 kwa hiyo waki-*convert* wakati huo mradi huo utafaidika zaidi kupata thamani ya mradi ule kwa wakati huo kuliko kuziweka katika *Tanzanian shillings. (Makofi)*

Na. 12

**Taarifa ya Viwavijeshi Nchini na Ununuzi wa Dawa za Kuwaangamiza**

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa tarehe 4/3/2006 Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, alitoa taarifa kwa umma juu ya kuwepo kwa mlipuko wa viwavi jeshi nchini, lakini kukawa na utata mkubwa kati ya taarifa iliyotolewa Wizarani kupitia barua ya Mtabiri wa Viwavijeshi kwa Katibu Mkuu yenye Kumb. Na. KI/PF/ 39097 ya tarehe 27/2/2006 kuhusu ombi la kustaafishwa kwa manufaa ya umma kwa sababu ya ubadhilifu wa fedha zilizopangwa kwa ajili ya viuatilifu kwa msimu wa 2004/2005 na 2005/2006 na kwamba utabiri wake kama mtaalum ulipuuzwa na wahusika kulindwa:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilitumika hadi mwisho wa mwaka wa fedha kutoka kwenye *Vote 43, Sub-vote 201* yenye shilingi 1,898,720,000 zilizoidhinishwa kwa mwaka 2004/2005 kama ilivyo kwenye kasma ndogo 2611229 *Insecticide* (*OC*) na katika kipindi hicho na hadi kufikia tarehe 13/2/2006 kulikuwa na milipuko mingapi, wapi kwa majina na ni fedha kiasi gani zimetolewa kutoka kwenye kasma ndogo kwa ajili ya *HQ* Kibaha, Morogoro, Arusha, Dodoma, Mbeya, Shinyanga, Kilimo Anga, *TPRI,* nje ya fedha zilizopelekwa baada ya mlipuko wa Desemba, 2005?

(b) Je, ni aina gani za dawa zimeagizwa nje ya nchi na ni waagizaji gani waliopewa leseni ya dawa hizo ikiwa uingizaji wake unasemakana ni *controlled* na kwamba taarifa ya Katibu Mkuu inaeleza kuwa dawa hizo zimenunuliwa ndani ya nchi, zenye namba zipi katika kipindi hicho hasa zilizo *import* viuatilifu hivyo?

(c) Kwa kuwa Katibu Mkuu katika taarifa yake ameeleza kuwa dawa hizo zimenunuliwa ndani ya nchi, je, Serikali inasema nini kuhusu leseni zilizotolewa na Wizara kuingiza dawa nchini mfano leseni yenye kibali Na. 446 Na.00000446 kati ya tarehe 21/2/2005 na tarehe 21/8/2005 na dawa hizo zilipelekwa kwenye Mikoa ipi kwa mgao gani kati ya kipindi kipi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mbunge wa Jimbo la Karatu, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka wa 2004/2005 jumla ya shilingi 1,896,724,100 zilitengwa kwa ajili ya kununua viuatilifu ili kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea ikiwa ni pamoja na nzige wekundu, viwavijeshi, kweleakwelea, panya na panzi kunuka. Kwa bahati nzuri katika msimu wa mwaka 2004/2005, milipuko ya viwavijeshi haikuwa mikubwa kama ilivyotabiriwa. Kwa hiyo, Wizara ilitumia shilingi 1,412,319,105 kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya mimea. Kati ya fedha hizo shilingi 770,430,969 zilitumika kununua viuatilifu, shilingi 10,000,000 zilitumika kununua mafuta ya ndege, shilingi 330,439,400 zilipelekwa katika vituo vya sehemu ya afya ya mimea Dodoma, Mbeya, Shinyanga, Arusha,*TPRI Bio Control* - Kibaha na *Rodent Control Centre* - Morogoro. Aidha, shilingi 301,448,735.9 zilitumika Makao Makuu ya Wizara kwa ajili ya kuratibu na kuendesha operesheni za udhibiti wa visumbufu. Shilingi 484,404,995 zilizobaki zilitumika kukamilisha michango ya mwaka 2004/2005 kwa shirika la kudhibiti nzige wa Jangwa la Afrika Mashariki na shirika la kudhibiti nzige wekundu la Afrika ya Kati na Kusini ambayo nchi yetu ni mwanachama.

Hadi kufikia tarehe 13/02/2006 jumla ya milipuko 26 ya viwavijeshi ilikuwa imetokea katika Mikoa ya Mbeya (Mbarali, Kyela, Rungwe, Ileje, Mbozi, Mbeya Mjini, Chunya, Mbeya Vijijini, katika Mkoa wa Iringa vilitokea (Ludewa, Iringa, Kilolo, Njombe na Mufindi) katika Mkoa wa Ruvuma vilitokea (Mbinga, Namtumbo na Tunduru) na huko Morogoro vilitokea (Kilombero, Ulanga, Mvomero, Kilosa Morogoro Vijijini), katika Mkoa Dodoma (Kongwa) katika Mkoa wa Mtwara (Masasina Newala) na katika Mkoa Lindi (Nachingwea, Rungwa). Kwa kawaida fedha hupelekwa vituoni baada ya ununuzi wa viuatilifu kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, hakuna fedha zilizopelekwa vituoni kabla ya mwezi Desemba, 2005 kwa sababu taratibu za ununuzi wa viuatilifu zilikuwa hazijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006 Wizara ilitangaza zabuni za ununuzi wa viuatifilifu mbalimbali vikiwemo viuatilifu vya kudhibiti viwavijeshi na makampuni yaliyoshindwa na kutunukiwa zabuni ni kama ifuatavyo:-

(i) Viuatilifu aina ya *Chloropyriphos 48% EC* na *Chloropyriphos 24% ULV* vilitolewa na *Mukpar Tanzania Ltd.* tarehe 10/2/2006 na 18 Aprili 2006. *Deltamethrin 0.5% ULV* na *Chloropyriphos 48% EC* zilitolewa na *Bajuta Vet. Agro* tarehe 06/03/2006

na viuatilifu aina ya *Fenitrothion 50% EC* na *Diazinon 60% EC* vilitolewa na *Bytrade Tanzania Ltd.* tarehe 18/04/2006. Makampuni yote haya na viuatilifu vilivyotolewa vimesajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu haitoi leseni za kuingiza kiuatilifu nchini bali hutoa kibali cha kuingiza kiuatilifu nchini *(permit to import pesticide).* Kibali Na. 446 anachouliza Mheshimiwa Mbunge ni cha kampuni ya *Mukpar Tanzania Ltd.* ambacho kilitolewa tarehe 21/2/2005 kwa kipindi cha miezi sita yaani hadi tarehe 21/8/2005. Kibali hiki kinahusu uingizaji nchini wa lita 10,000 za kiuatilifu aina ya *Chloropyriphos 24% ULV.* Wizara yangu ilinunua lita 8500 tu za kiuatilifu hicho ambazo zilisambazwa kama ifuatavyo: Dodoma lita 1000 tarehe 19/6/2005, Mbeya lita 1000 tarehe 6/9/2005, Dodoma lita 1000 tarehe 31/10/2005, Singida, Tanga na Morogoro lita 500 kila Mkoa na zilitolewa tarehe 7/12/2005, Mbeya lita 1,000 tarehe 3/1/2006, Mtwara lita 400 tarehe 13/1/2006, Lindi lita 500 tarehe 13/1/2006, Mbeya lita 1000 tarehe 19/1/2006 Masasi lita 100 tarehe 26/1/2006 na lita 200 tarehe 28/1/2006.

Aidha, Shinyanga ilipewa lita 150 tarehe 31/1/2006, Morogoro lita 200 tarehe 1/2/2006, Iringa lita 50 tarehe 1/2/2006 na Rwangwa lita 100 tarehe 1/2/2006, Nachingwea ilipata lita 100 1/2/2006, Morogoro lita 40 tarehe 3/2/2006 na lita 100 tarehe 9/2/2006 na Dodoma lita 60 tarehe 20/2/2006.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali, aidha, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake marefu na yanayokidhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu hayo ningependa kupata ufafanuzi kwamba je, baada ya taarifa kutolewa kwamba kuna waliohusika kuuza hizo dawa kwa utaratibu usio wa kawaida kutoka kwenye ofisi yetu ya Kanda kule Arusha na taarifa ikapelekwa kituo cha polisi na kufunguliwa *RB USRIR 732/2006* na kesi hiyo baadaye kupelekwa mahakamani, je, Serikali inatoa taarifa gani kwamba uhalifu huo upo au haupo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza yeye mwenyewe amesema suala hilo litapelekwa polisi na linashughulikiwa. Sasa kama linashughulikiwa basi tusubiri hayo majibu ya mahakama halafu tutaweza tukalizungumza. Lakini sasa itakuwa si muda muafaka kulizungumza kama liko mahakamani. (*Makofi*)

Na. 13

**Kilimo cha Mashamba Makubwa**

**MHE. MARIA IBESHI HEWA** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala zima la kukosekana kwa mvua endelevu hasa na ukataji hovyo wa miti hasa katika maeneo ya kilimo cha mashamba makubwa *(estates)* ya Katani/Mkonge, Nanasi, Pamba na kadhalika yaliyomo nchini:-

(a) Je, Serikali ina maandalizi gani ya kitaalam kujua ni miti gani inapaswa kupandwa katikati *(between rows)* ya mistari ya mazao ili yaweze kustawi na miti kwa pamoja bila kuathiri mwingine?

(b) Je, Serikali ina wataalam wangapi wanaotasheleza hitaji la nchi wenye taalam ya kujua ni miti gani inayofaa kwenye udongo fulani na kama wapo wako Mikoa gani.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna uhusiano mkubwa kati ya misitu na mvua kwani misitu inahifadhi maji ndani ya ardhi na pia hutoa mvuke hewani kupitia mfumo ujulikanao kama *Evapo Transpiration* na mvuke huu ndiyo chanzo cha mawingu yanayoleta mvua. Aidha, misitu hupunguza kasi ya upepo na kuwezesha kutulia kwa mawingu na hatimaye mvua kupatikana na hii ndio sababu maeneo mengi yenye misitu ndiyo yanapata mvua za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba makubwa ya katani, pamba mananasi na mengineyo hayana athari ya moja kwa moja kwa mazingira. Uharibifu wa mazingira hutokea kupitia ukataji wa miti na mimea mingine bila kuchukua hatua mahsusi za kutunza ardhi na vyanzo vya maji katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Maliasili na Utalii na vyuo vya utafiti ambavyo pamoja na shughuli zingine hutafiti suala zima la kilimo mseto *(Agro Forestry)*. Kwa mfano, kituo cha utafiti cha Tumbi huko Tabora kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Utafiti wa Kilimo Mseto (*ICRAF*) kimekuwa kikifanya utafiti wa miti kwenye mazao hasa ya mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti umeonyesha kuwa mahindi yakipandwa kati ya miti aina ya miakasia *(Acacia species) Migrilicidia* na *Grilicidia spp* na pia Milusina *(Leucaena species)* haiathiri uzalishaji wa mazao kama ikipandwa na kutunzwa kwa kufuata utaalam. Miti hii imefanyiwa utafiti na ikaonekana ina uwezo mkubwa wa kurutubisha udongo na kusaidia kuhifadhi unyevunyevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mashamba makubwa ya katani, pamba na mananasi inashauriwa kupanda miti kwenye mipaka ya mashamba. Miti inayopandwa inategemea uoto wa asili na hali ya hewa, kwa mfano, katika ukanda wa magharibi ambako hali ya hewa ni ya joto na uoto ni wa miombo, miti inayofaa kupandwa ni pamoja na *Senna species*, *Grevillea species, Leucaena species* na miti ya kienyeji kama vile mizima, na kadhalika.

Vile vile Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inahimiza wakulima wa tumbaku kuwa na mashamba ya miti itakayotumika kukaushia tumbaku badala ya kukata miti kwenye misitu na kuharibu mazingira.

Aidha, baadhi ya makampuni yanayonunua tumbaku yamejiwekea utaratibu na wakulima, ambapo mkulima anatakiwa kuwa na shamba la miti ya kukaushia tumbaku kabla ya kuingia mkataba wa kukopeshwa pembejeo na kuuza tumbaku yake.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina wataalam 53 katika Kanda zake za utafiti chini ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika Tanzania Bara, kama ifuatavyo:-

Kanda ya Mashariki yenye Mikoa ya Morogoro, Pwani na Dar es Salaam wataalam 23, Kanda ya Kaskazini (Arusha, Tanga, Manyara na Kilimanjaro) wataalam 6; Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yenye Mikoa ya Mbeya, Rukwa, Iringa na Ruvuma watalaam 7, Kanda ya Ziwa yenye Mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara na Shinyanga wataalam 8; Kanda ya Magharibi yenye Mikoa ya Tabora na Kigoma wataalam 4; Kanda ya Kusini yenye Mikoa ya Mtwara na Lindi na Kanda ya Kati yenye Mikoa ya Dodoma na Singida wataalam 2.

**MHE. MARIA IBESHI HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongeze kuuliza swali moja tu kutokana na majibu mazuri ya Naibu Waziri jinsi alivyojibu swali langu. Ninachotaka kusema ni kwamba yeye mwenyewe amekiri kwamba kunahitajika miti ambayo inaweza kunusuru suala zima la mashamba haya ambayo kwa kweli yako wazi na yanatutia aibu.

Je, ni lini Serikali kama sisi itakuwa na mikakati ya kuweza kuhamasisha upandaji walau wa miti ambayo itapandwa misitu mizito kuzunguka mazao hayo, yeye kataja tumbuku tu. Je, kwenye mkonge, pamba na mashamba mengine ili tuweze kunusuru janga la ukosefu wa miti kuzunguka haya mashamba ambayo ukipita barabarani kwa kweli unaona aibu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nakubaliana kabisa na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na hivi sasa tayari Serikali imekwishaanza mikakati hii siyo kwamba Serikali haijaliona hili, ndiyo maana katika mazao mengine kama tumbuku nimeeleza kwamba kuna mikakati hiyo, baadhi ya makampuni yameanza utaratibu kuwafanya wakulima kuwapa motisha ya kupanda miti. Kwa hiyo, katika mashamba haya ambayo tukipita tunayaona ni wazi Serikali inaliona hilo na ndio maana tayari tumeweka hata katika vituo vyetu vya utafiti kutafiti aina ya miti hasa inayofaa. Tunajua utafiti unachukua muda mrefu takribani miaka mitano. Lakini nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba suala analolisema ni suala la uhakika kabisa na ni suala ambalo Serikali italifanyia kazi.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuzwa swali kuhusu upandaji wa miti. Waziri amekiri

kwamba kuna mahusiano mazuri kati ya miti na mvua na katika jibu lake la msingi ameeleza kwamba katika Kanda ya Ziwa hasa Mwanza kuna watalaam wanne tu. Je, Serikali haioni kwamba watalaam hawa ni wachache na hawatoshi na ukizingatia kwamba tunataka kupanda miti ambayo itakubaliana miti ambayo haiathiri pamba na miti ambayo haitaingiliana na wakataji wanaotumia mkaa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba wataalam ni wachache lakini hiyo inatokana na uchache wenyewe na hali ya upatikanaji wa watalaam na hali ya kifedha tuliyokuwa nayo Serikalini. Lakini sasa hivi hali inaendelea kuboreka na tunaendelea kuomba vibali vya kuajiri watalaam na nina hakika muda ujao watalaam wataongezeka. *(Makofi)*

Na. 14

**Waandishi wa Habari Waliopigwa na Kuvunjiwa Vyombo Vyao**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa Waandishi wa Habari ni watu muhimu sana kwa maisha ya watu na maendeleo ya nchi kwa sababu wana kazi ngumu ya kufanya utafiti wa kina na baadaye kuelimisha jamii kwa kutoa habari mbalimbali na kwa kuwa wakati wa kipindi cha harakati za uchaguzi wa mwaka 2005 kuna waandishi wa habari ambao walinyanyaswa kwa kupigwa na hatimaye kuvunjiwa na kunyang’anywa vifaa vyao vya kazi, kitendo ambacho ni uvunjaji wa haki za binadamu:-

(a) Je, Serikali iliwachukulia hatua gani wale waliobainika kuwapiga waandishi wa habari?

(b) Je, ni fidia gani walipewa wale waandishi waliopigwa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli wakati wa kipindi cha Uchaguzi wa mwaka 2005 baadhi ya Waandishi wa Habari walinyanyaswa kwa kupigwa na hatimaye kuvunjiwa na kunyang’anywa vifaa vyao vya kazi na baadhi ya wafuasi wa Vyama vya Siasa. Hata hivyo, Serikali ilichukua hatua za harakati za kuwakamata wale wote waliotuhumiwa kufanya vitendo hivyo vya uhalifu na kuwafikisha Polisi.

(b) Hakuna fidia iliyotolewa kwa waandishi hao waliopigwa. Serikali inatoa wito kwa Vyama vya Siasa, kuwaelimisha na kuwadhibiti wanachama na wafuasi wao ili

wasiwabugudhi Waandishi wa Habari wakati wakiwa kazini kwa vile ni watu muhimu kwa maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Vile vile Waandishi wa Habari wanapewa changamoto ya kujenga mahusiano mazuri na Vyama vya Siasa na kuendelea kuzingatia maadili ya taaluma zao. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kumwuliza hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba ni wafuasi wa Vyama vya Siasa ndivyo vilivyowadhalilisha Waandishi wetu wa Habari. Naomba kujua tu ni wafuasi wa chama gani hicho na madhara gani zaidi yalipatikana zaidi ya hayo? Na Serikali inatoa kauli gani leo hapa kwa wafuasi hao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali namba mbili. Kwa kuwa imedhihirika kuwa Waandishi wetu wa Habari wapo katika mazingira ya hatari katika utendaji wa kazi zao za kila siku. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa waajiri wao kuwapatia au kuwatengenezea bima ya ajali na maisha? Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MICHEZO NA UTAMADUNI (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza katika mchakato wa uchaguzi, chama kilichotuhumiwa kufanya hivi ilikuwa Chama Cha Wananchi *(CUF)* katika tukio lililotokea katika wiki ya kwanza ya mwezi Novemba wakati walipowaalika Waandishi wa Habari kwenye mkutano na bahati mbaya walipofika maeneo yale wakafanyiwa vurugu na kujeruhiwa. Chama cha Wananchi *(CUF)* kilieleza kusikitishwa na tukio hilo.

La pili, kauli ya Serikali katika jambo hili ni kuwataka wadau wote wa habari kutambua nafasi ya vyombo vya habari kwa maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, tushirikiane kuwatunza, kuwaenzi na kufanya nao kazi kwa faida ya nchi yetu.

Kuhusu umuhimu wa kuwapa bima Waandishi wetu wa Habari, tunatambua umuhimu wa kuwapa bima. Lakini jambo la msingi kwa sasa kwa Serikali ni kuhakikisha wanafanya kazi katika mazingira salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutafanya wajibu wetu huo wa kuhakikisha kwamba wanafanya kazi katika mazingira salama na wakati huo huo tutaendelea kushauriana na wadau kuhusu namna bora zaidi ya kuhakikisha kwamba wakipata madhara hawapati maafa makubwa. Ahsanteni sana.

Na. 15

**Tatizo la Maji Kilombero**

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mji wa Ifakara na Mlimba Wilayani Kilombero kuna tatizo sugu la upatikanaji wa maji kutokana na matumizi makubwa ya umeme unaotumika kupampu maji na kwa kuwa miji hiyo ina vyanzo mbadala vya kutega maji kwa *gravity* kutoka milimani yaani sehemu ya Kiburubutu - Nanganji na Mto Lumemo kwa mji wa Ifakara na mto Mpanga kwa mji wa Mlimba:-

Je, Serikali itakubali kuingiza miradi hiyo miwili kwenye mpango wa mwaka 2006/2007 ili kupunguza gharama za upatikanaji wa maji katika miji hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Castor Ligallama, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo, Mji wa Ifakara unapata huduma ya maji kutoka kwenye visima virefu vitano ambavyo maji yake husukumwa kwa kutumia nishati ya umeme. Aidha, mji mdogo wa Mlimba nao unapata huduma ya maji kutoka kwenye visima vitatu ambavyo maji yake husukumwa kwa kutumia nishati ya umeme. Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa gharama za uendeshaji ni kubwa na ni kweli kuwa kuna chanzo kingine cha maji kilichopo katika Milima ya Udzungwa Kiburubutu ambacho kinaweza kutega maji kwa mtiririko *(gravity)* kwenda katika mji wa Ifakara.

Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa mji wa Ifakara na Mlimba ni miongoni mwa vijiji kumi ambayo imepitishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero kuingia katika Programu ya Kitaifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ambayo utekelezaji wake unaanza katika mwaka wa fedha 2006/2007. Utekelezaji wa programu hii utaanza kwenye ukarabati wa miradi iliyopo na ujenzi wa miradi mipya midogo midogo ambayo inalenga kupunguza kero ya maji kwa wananchi haraka *(quick wins)*. Wakati huo huo mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali *(NGOs)* na Makampuni ya ushauri wa kitaalam *(Consulting Firms)* yatakuwa yanaendelea na shughuli za uhamasishaji na maandalizi ya miradi katika miji na vijiji kumi kati ambavyo viwili ni Mlimba na Ifakara vilivyochaguliwa kujiunga katika awamu hii. Mtaalam Mshauri *(Consultant)* atashirikiana pamoja na wataalam wa Wilaya ya Kilombero na wakazi wa Ifakara na Mlimba, ili waweze kuainisha kama maji ya mtiririko *gravity* kutoka mlimani yanaweza kutosheleza mahitaji ya maji kwa wakazi wa Mji wa Ifakara na Mlimba.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Sina swali la nyongeza.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba vijiji 10 katika hii Wilaya vinaingizwa moja kwa moja kwenye mradi wa Taifa wa Maji Safi Wilaya, vinaingizwa moja kwa moja kwenye mradi wa

Taifa wa Maji Safi ambao unaingia kwenye Bajeti inayokuja na kwa kuwa kama niko sahihi mradi huu ni mradi mkubwa kabisa wa *World Bank* ambao umeenea nchi nchi nzima ambako kila mwaka Wilaya inaruhusiwa kuwa na vijiji 10 vinavyoingia kwenye ule mradi.

Namwomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri ni kitu gani kinafanya miradi hii ya Benki ya Dunia nchi nzima ikiwa na pamoja na Singida Kaskazini kusuasua kuchukua muda mrefu kuleta longolongo kiasi kwamba wananchi ambao wamechangia miradi hii wamefika mahali wamekata tamaa na wanataka maswali yao juu ya hii miradi yajibiwe ni lini miradi hii itafanikiwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:**Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu unaofuatwa na Benki ya Dunia hapo nyuma ulikuwa ni kwamba tunapopata *Consultant* na kufanya upenguzi yakinifu miradi hii ilikuwa ikiendeshwa lakini fedha na ripoti zake zilikuwa zinawasilishwa mpaka Benki ya Dunia kabla fedha hazijatolewa. Utaratibu ulikuwa unachelewesha utekelezaji.

Sasa hivi utaratibu huu umebadilika. Benki ya Dunia itatoa fedha zitakuwa ziko Hazina.

Kwa hiyo, taarifa zote zitakazokuwa zinatolewa zitakuwa zinatolewa malipo kwa haraka zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma. Kwa hiyo, ninachoweza kusema hapa ni kwamba kuanzia mwaka wa fedha 2006/2007 na chini ya utaratibu huu ambao Hazina itakuwa ina fedha na malipo kutolewa mapema zaidi badala ya kupeleka taarifa Benki ya Dunia Washington utatuwezesha kwenda kwa haraka zaidi na kwa hiyo, napenda kutumia nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kushirikiana na Wizara yangu na Halmashauri za Wilaya kutambua miradi ile mahali popote ilipo na kuwa na mawasiliano nasi mahali panapoonekana inachelewa ili tuhakikishe ya kwamba inafanyaka kazi na kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuwapatia wananchi wengi zaidi maji kupitia programu hii. *(Makofi)*

Na. 16

**Tatizo la Maji - Tarime**

**MHE. CHACHA Z. WANGWE** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1995 Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu aliwaahidi wananchi wa Tarime kwamba Serikali itawaondolea tatizo na adha ya kukosa maji kwa kuhakikisha inapeleka maji mjini Tarime na viunga vyake:-

Je, Serikali inatarajia kutekeleza ahadi hiyo lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mbunge wa Tarime, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mji wa Tarime una idadi ya watu wapatao 30,937 kulingana na sensa ya mwaka 2002. Mahitaji ya maji kwa mji huo kwa sasa yanakadiriwa kuwa mita za ujazo 4,200 kwa siku. Kwa sasa mji wa Tarime unapata huduma ya maji kutoka kwenye chemchem ya Nyandurumo, pia bwawa la Tagota pamoja na visima vifupi vichache vilivyopo mjini humo. Vyanzo hivi kwa pamoja vinakadiriwa kuwa na uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 2,000 kwa siku. Kwa hali hiyo, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa hali ya sasa maji hayatoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutekeleza ahadi ya mwaka 1995 ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Katika mwaka 2003/2004 utafiti wa maji chini ya ardhi ulifanyika katika maeneo ya mji wa Tarime kwa lengo la kupata maeneo ya kuchimba visima. Matokeo ya utafiti huo yameonyesha kutokuwepo maji mengi chini ya ardhi katika mji wa Tarime.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2004/2005 ulifanyika upembuzi yakinifu kwa lengo la kuainisha chanzo cha maji ya kutosha kuboresha huduma ya maji katika mji wa Tarime. Usanifu wa awali wa mradi wa maji kwa kutumia mto Mori ulikamilika. Jumla ya shilingi milioni 25 zilitumika kwa kazi hiyo. Pia kiasi cha shilingi milioni 35 zaidi zilitumika kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji kwa lengo la kuboresha huduma hiyo kupunguza kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua inayofuata na ambayo itatekelezwa na Serikali yangu katika mwaka wa fedha 2006/2007 ni kufanya usanifu wa kina, kabla hatua za utekelezaji hazijachukuliwa.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwanza Tarime ni moja ya Wilaya za zamani sana hapa nchini, lakini kuna Wilaya nyingi ambazo zimepata huduma ya maji ambazo ni Wilaya za hivi karibuni. Je, Serikali inatumia *criteria* gani inapokuwa inaamua kupeleka maji katika miji na Wilaya mbalimbali nchini? *(Makofi)*

Pili, mji wa Tarime uko karibu sana na Ziwa Victoria chanzo cha Mto Mori ni chanzo ambacho mto ule unakauka kila mara. Je, Serikali haioni ya kwamba ingekuwa ni gharama nafuu kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria ili iweze kukidhi mahitaji ya Wilaya ya Tarime kwa ujumla?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mwenyewe labda anajua huko Tarime. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umri au muda gani Wilaya imekuwepo siyo hasa la msingi. Kwa sababu Wilaya zote nchini zimewahi kupata huduma ya maji. Kinachotokea ni kwamba ongezeko la watu linafanya kiwango cha maji kinachokuwa kimetolewa katika Wilaya hizo kupungua na hivyo ndivyo hali ilivyo katika Wilaya ya Tarime. Huduma ya maji ilitolewa katika siku zilizopita lakini idadi ya watu katika mji wa Tarime imeongezeka na kwa hiyo, mahitaji zaidi ya maji yanatakiwa kuliko vile huduma ilivyokuwa imewekwa katika siku zilizopita. Na kwa kuzingatia msingi huo ndiyo maana tunachukua hatua ya kutaka kuweka huduma kubwa zaidi ya maji kulingana na mahitaji ya watu katika mji wa Tarime.

Swali la pili kuhusu kuchukua maji kutoka Ziwa Victoria. Mara nyingi sana tunafanya uamuzi kwa kutegemea gharama. Mto Mori unapita karibu sana na Mji wa Tarime na mimi siku chache zilizopita mwezi huu nilitembelea mji wa Tarime pamoja na chanzo cha maji ambacho kinakusudiwa kutumiwa kuleta maji katika mji wa Tarime. Niliridhika ya kwamba mto ule unaweza kuwa chanzo kizuri na hasa tukijenga bwawa dogo ambalo linakinga maji kwa kutumia *gravity* yanakwenda kwa mtiririko kuliko kutoa maji Ziwa Victoria ambayo yatataka kupampu ambayo inaingiza gharama kubwa.

Kwa hiyo, kama kuna uwezo wa kuweka maji pale kwa gharama nafuu mimi nadhani gharama nafuu ni nafuu kuliko gharama kubwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ningependa tuendelee lakini muda hautoshi. Tunaingia Wizara ya Miundombinu.

Na. 17

**Tanzania na Uanachama wa *IMO***

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni mwanachama wa *International Maritime Organization (IMO)*:-

(a) Je, ni faida gani Tanzania inazipata kwa kuwa mwanachama wa *IMO?*

(b) Je, ni hasara gani zingepatikana kama Tanzania isingekuwa mwanachama wa *IMO?*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa mwanachama wa *IMO,* Tanzania inanufaika kama ifuatavyo:-

(i) Kuwa na Sheria zinazotoa mwongozo wa namna ya kushughulikia na kuboresha usalama na usafiri wa majini, kuendesha shughuli za usafiri wa majini kwa viwango vya Kimataifa na hivyo kuvutia wawekezaji;

(ii) Kuwa na mabaharia wa Kitaifa wanaotambulika Kimataifa na hivyo kuweza kupata ajira kwenye meli za kigeni;

(iii) Kuwa na fursa ya kushirikiana na kuwa na makubaliano ya pamoja kati ya nchi jirani ili kusaidiana kiufundi na kwa nyenzo katika utafutaji na uokoaji endapo kutatokea janga lolote kwenye maji yetu;

(iv) Wataalamu wetu wanapata mafunzo na uzoefu mbalimbali katika usafiri wa majini kwa kupitia programu mbalimbali zinazoratibiwa na Shirika hili na katika kuhudhuria mikutano ya Kimataifa ya usafiri wa majini; na

(v) Chuo chetu cha Mafunzo ya Ubaharia cha *Dar es Salaam Maritime Institute (IDM)* sasa kinatambulika Kimataifa na hivyo kuweza kutoa elimu kwa nchi nyingine.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya hasara ambazo zingepatikana iwapo Tanzania isingekuwa mwanachama wa *IMO* ni kama ifuatavyo:-

(i)) Mabaharia wa Tanzania wasingetambuliwa Kimataifa na hivyo kukosa ajira.

(ii) Meli za Kimataifa zisingekuja kwenye bandari zetu kwa kutokukidhi viwango vya Kimataifa vya kibandari.

(iii) Tusingeweza kupata misaada kutoka kwenye nchi nyingine ambazo ni wanachama wa *IMO* katika nyanja mbalimbali zikiwemo masuala ya utafutaji na uokoaji na katika kupata fidia iwapo meli ya nchi nyingine itamwaga mafuta kwenye bahari yetu na kuchafua mazingira.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa vile usafiri wa baharini si suala la Muungano. Tanzania ilitumia kigezo gani, ilifuata sheria zile za Zanzibar au sheria za Tanzania Bara ili kuwa *registered* katika *IMO* na kwa maana hiyo je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi sasa kuisaidia Zanzibar ili kupata *associate membership?*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, kwamba ili tuingie katika masuala ya Kimataifa ni lazima

nchi yoyote ihusike na Sheria ya *Merchant Shipping Act.* *Merchant Shipping Act* ndiyo inayotumika Kimataifa na Zanzibar tulishirikiana nao kabisa wakati tunatunga sheria hii kikamilifu na sidhani kama Tanzania imekwenda kinyume na taratibu ambazo zimewekwa. Kama Zanzibar ingependa kuwa *associate member* hilo ni suala la kwenda kuomba *IMO,* Tanzania tuko tayari kuwasikiliza wakitaka msaada kwetu.

Na. 18

**Ujenzi wa Barabara ya Korogwe - Mikumi**

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ya kuwashukuru wakazi wa Dodoma hapo tarehe 9/2/2006 aliendelea kuisisitizia Serikali kuhakikisha kwamba, inatekeleza ahadi zilizotolewa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na kwa kuwa moja kati ya ahadi hizo ilikuwa ni ujenzi wa barabara ya Korogwe - Handeni - Turiani hadi Mikumi kwa kiwango cha lami:-

(a) Je, Serikali inaweza kuliarifu Bunge na wananchi wa maeneo hayo kwamba utekelezaji wa mradi huo hadi sasa umefikia wapi?

(b) Je, Serikali inaona umuhimu wa barabara hiyo hasa kiusalama, kiuchumi na vile vile kupunguza gharama kwa wawekezaji kwa ujumla, hivyo ione haja ya kuijenga kwa haraka?

(b) Je, ni ratiba gani ya utengenezaji wa barabara hiyo imewekwa na Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Korogwe - Mkata - Turiani hadi Mikumi yenye urefu wa jumla ya kilometa 434 ni barabara muhimu inayounganisha sehemu za Mashariki na Kati kuelekea Kusini Magharibi na Kaskazini Magharibi mwa nchi yetu. Barabara hii mbali na kuwa yenye manufaa kiuchumi, pia ni fupi kutoka Korogwe kuyafikia maeneo yaliyotajwa hivyo kupnguza gharama za usafirishaji.

Kwa sasa barabara hii ni ya kiwango cha changarawe na udongo na inapitika kwa mwaka mzima, licha ya kuwepo maeneo korofi yanayopitika kwa shida wakati wa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, barabara hii ni moja ya barabara zilizoainishwa kuanza kufanyiwa upembuzi yakinifu na

usanifu ili hatimaye zijengwe kwa kiwango cha lami. Aidha, mradi huu ni moja ya ahadi za Mheshimiwa Rais kujengwa kwa lami ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua za muda mfupi, maeneo yote korofi yanayosababisha barabara hizi kutopitika vizuri hasa wakati wa mvua yatakarabatiwa kwa kiwango cha changarawe chini ya mpango wa *Road Sector Programme Support (RSPS) Phase III* wa *DANIDA* na *Performance Based Maintenance and Management of Roads (PMMR)* wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya barabara itakayohusika na mpango wa *DANIDA* kwa Mkoa wa Morogoro ni kutoka Mziha - Magole kilometa 88 na awamu ya kwanza ya mradi huu itahusisha sehemu ya barabara ya Mziha - Turiani ambayo ni kilometa 45. Jumla ya shilingi 442 milioni zitatumika katika mpango huu wa Awamu ya Kwanza iliyoanza Agosti 2005 na kutarajiwa kukamilika Januari 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili, itahusisha sehemu ya Turiani kwenda Magole yenye kilometa 43. Aidha, kwa upande wa Mkoa wa Tanga itahusisha sehemu ya barabara hiyo kuanzia Handeni hadi Mziha yenye kilometa 70 ambayo itafadhiliwa na *DANIDA* kwa gharama ya fedha za Denmark milioni sita na nusu na Handeni hadi Korogwe kilometa 66 itakuwa chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia mpango wa *Performance Based Maintenance and Management of Roads* na jumla ya shilingi milioni 588.2 zitatumika. Kazi za ukarabati zinategemewa kuanza kuanza mwaka wa fedhas 2006/2007 mwezi Julai kwa barabara ya Korogwe kwenda Handeni na mwezi Novemba kwa barabara ya Handeni kwenda Mziha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua za kuijenga barabara hii kwa lami na kwa hiyo kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM Serikali tayari imeanza utaratibu wa kuifanyia upembuzi yakinifu barabara hii kwa awamu na jumla ya shilingi milioni 302.5 tayari zilishatengwa kwa kazi hii. Zabuni ya kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kazi hii imetangazwa na kazi ya uchambuzi zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii itaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2006/2007 kutoka Magole kwenda Kilosa hadi Mikumi. Lakini kwa sehemu ya barabara inayoanzia Magole-Turiani-Mziha-Handeni upembuzi yakinifu umekwishagharamiwa na *DANIDA* katika mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu Serikali itaendelea na hatua ya pili ya kufanya usanifu wa kina na nafasi itakayoweza Serikali kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi.

Na. 19

**Tofauti ya Malipo ya Uzeeni kwa Askari Polisi**

**MHE. AMEIR ALI AMEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkataba wa *Police General Order* unaoongoza Jeshi la Polisi Tanzania umeandikwa tangu wakati wa ukoloni na sasa hivi unaonekana kupitwa na wakati na unaleta ubaguzi kwa askari hasa wakati wa kustaafu kwenye malipo ya pensheni na kiinua mgongo, ambapo wale askari ambao ni *pensionable* hulipwa mafao makubwa na kila baada ya miezi sita pia hulipwa mafao ya uzeeni tofauti na askari wale wanaolipwa kiinua mgongo ambao hulipwa mafao madogo sana:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa inafanya ubaguzi, uonevu na dhuluma ya hali ya juu kwa askari wa nchi moja, walikwenda depu pamoja na wakati mwingine kupandishwa vyeo wakati mmoja lakini malipo yao ya kustaafu yanatofautiana kiasi hicho?

(b) Je, Serikali haioni kuwa hao askari wanaostaafu na kulipwa kiinua mgongo wanakuwa kwenye umaskini mkubwa zaidi?

(c) Je, Serikali haioni kuwa sasa umefika wakati kwa kuufuta mkataba huo na badala yake askari wote wawe na mkataba mmoja wa pensheni?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kanuni za jumla zinazoongoza utendaji kazi kwa Jeshi la Polisi nchini zimeandikwa katika kitabu kinachoitwa *Police General Orders (POG)* ambacho kilianza kutumika kabla ya nchi yetu kupata Uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni, amri na miongozo iliyomo katika *PGO* huboreshwa kila inapolazimu kufanya hivyo kwa kutumia amri za utendaji zinazotolewa na Inspekta Jenerali wa Polisi. Kanuni hizo zinatolewa mara kwa mara zinaitwa amri za Kijeshi *(Force Operational Orders)*. Aidha, taratibu za utumishi zimeundiwa mwongozo, yaani *Police Force Service Regulations* za mwaka 1995.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, siyo sahihi kusema kwamba Serikali inafanya ubaguzi, uonevu na dhuluma ya hali ya juu kwa askari polisi nchini wakati wa kuwalipa mafao yao ya kustaafu. Kila askari mstaafu hulipwa stahili ya mafao yake ya kustaafu kulingana na vigezo maalum ikiwa ni pamoja na kuzingatia masharti ya utumishi *(Terms of Service)* aliyoyachagua yeye mwenyewe kwa hiari yake baada ya kutimiza utumishi wa miaka 12 mfululizo katika Jeshi la Polisi. Mafao ya kustaafu kwa Askari Polisi kama

walivyo watumishi wengine wa Serikali yalikuwa yanalipwa na Hazina hadi mifuko ya *GEPF* na *PSPF* ilipochukua jukumu hilo kuanzia mwezi Julai, 2004.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba askari polisi ambao mafao yao yanaongozwa na masharti ya malipo ya bakshishi *(Gratuity)* wanapostaafu wamekuwa wakilipwa mafao ya kiinua mgongo ambayo ni kidogo ukilinganisha na wale wanaomilikiwa na malipo ya uzeeni *(Pensionable).* Kama nilivyoeleza katika sehemu (a) ya jibu langu na kwa kurejea *PGO* kifungu Na. 48 (2), uchaguzi wa kuendelea kufanya kazi kwa mkataba wa miaka mitatu na malipo ya bakshishi *(gratuity)* hufanywa na askari mwenyewe kwa hiari yake baada ya kuelimishwa na viongozi wake kuhusu faida na hasara ya kila chaguo.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari anayechagua kufanya kazi kwa mkataba wa malipo ya bakshishi *(Gratuity)* huwa ameamini na kuridhika kwamba chaguo hilo ni bora kwa maslahi yake kuliko lile la kujiunga na masharti ya kudumu na pensheni. Baadhi ya askari hupenda kufanya kazi kwa mikataba ili wawe huru kuacha kazi wakati wowote wapendao na kulipwa kiinua mgongo chao.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkutano wa Bunge uliopita Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia alizungumza na askari wa mji wa Dodoma na tulibaini kuwa hii ni kero kubwa miongoni mwa askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali ipo katika mchakato wa kuirekebisha *PGO* katika ujumla wake ili askari wote waweze kulipwa mafao yaliyo bora na suala hili ni miongoni ya masuala yatakayofanyiwa marekebisho ili jeshi liwe na utaratibu mmoja wa pensheni.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa lengo la Serikali ni kuinua hali ya maisha ya wananchi wake na kwa kuwa imebainika kwamba wako askari wale ambao wakishapata kiinua mgongo hawana malipo ya aina yoyote na bado wanaishi. Je, katika hayo mabadiliko hamwoni kwamba sasa ni wakati muafaka wa Serikali kuwafikiria askari kama hao waliokuwa hawapati chochote na kuwafikiria kupata chochote baada ya mabadiliko?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba uchaguzi wa kuamua ni aina gani ya ustaafu wake kama ni pensheni au kiinua mgongo ni suala la askari mwenyewe na kwa kuwa uamuzi huo unafanywa na askari mwenyewe kujua faida na hasara zake. Kama tulivyosema kwamba sasa tutajitahidi tuuweke utaratibu mpya ambao utawafaa askari wote ili tusipate malalamiko ya aina hii.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaongeza dakika tatu kwa sababu tulitumia muda kutangaza pale mwanzo, kwa hiyo namwita Mheshimiwa Mkiwa Kimwaga, ili aulize swali lake.

Na. 20

**Mapambano kati ya Mgambo na Machinga**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa mapambano ya kukabiliana kwa mawe na virungu vya mgambo wa Jiji la Mwanza na wamachinga yalianza kama mzaha siku zilizopita na kwa kuwa hali hiyo inaongezeka sana kiasi kwamba tarehe 7 Machi, 2006 mgambo hao waliwavamia wamachinga na kuwanyang'anya mali zao na hali hiyo ilitaka kusababisha vita, hali ya kutokuwa na usalama, mali za watu kuwa hatarini, kutumika kwa risasi za moto, mitaa na maduka kufungwa, magari kuvunjwa vioo na madhara mengineyo:-

(a) Je, Serikali haioni vema kuweka utaratibu mzuri na maafikiano badala ya mapambano na wamachinga?

(b) Je, kwa kuwa Serikali ndiyo iliyoanzisha vurugu kupitia mgambo wa Jiji la Mwanza na kusababisha uharibifu mkubwa, je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia wananchi waliopata hasara na pia kurudisha mali za wamachinga hao?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA NA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama na Uraia, kumjibu Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali siku zote inapenda kuona utaratibu mzuri wa maafikiano badala ya mapambano na wafanyabiashara wadogo wadogo (wamachinga) na ndio maana kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Maendeleo ya Miji Na.8 ya mwaka 1982 kifungu cha 59), kinazipa uwezo wa kisheria Halmashauri kudhibiti uendeshaji wa biashara kwenye mitaa na masoko yaliyoanzishwa rasmi mijini.

Hata hivyo, kwa kuona umuhimu wa majadiliano, Halmashauri ya Jiji la Mwanza imekuwa ikifanya majadiliano na wafanyabiashara ndogo ndogo kwa muda mrefu tangu mwaka 2002 na pande mbili hizi ziliafikiana na wafanyabiashara hao kujenga kwa gharama zao sehemu za kufanyia biashara katika maeneo ya Buzuruga, Kiloleni, Mabatini , Kitangiri, Sabasaba na Temeke.

Hata baada ya ujenzi huo kukamilika wafanyabiashara hao hawakuhamia kwenye maeneo husika kwa madai kuwa hapakuwa na huduma za vyoo. Halmashauri iliboresha masoko hayo lakini bado walipinga kuhama kwa kutoa madai mpaya mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, si vyema kwa wananchi kutotii sheria na kuchukua hatua mikononi mwao, kitendo ambacho husababisha vurugu na kuhatarisha usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu naomba kutoa wito kwa wale wenye tabia ya kujichukulia sheria mikononi mwao, kuacha tabia hiyo mara moja na kufuata mkondo wa sheria ili waweze kufanya shughuli zao bila bugudha na bila kubugudhi wengine.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haikuanzisha vurugu kupitia wana mgambo wake, bali vurugu zilianzishwa na baadhi ya wamachinga na baadhi ya watu wengine waliokuwa jirani eneo hilo. Aidha, imebainika kuwa hakuna mali za wamachinga zilizoporwa na wanamgambo wa Jiji, badala yake baadhi ya wamachinga na baadhi ya watu waliokuwa jirani eneo hilo ndio walioanzisha uporaji wa mali za wafanyabiashara baada ya kuvunja madirisha, milango ya maduka na majengo ya biashara. Hivyo Serikali haina mpango wa kulipa fidia kwa vile haiusiki na uharibifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kutoa wito kwa wale wenye tabia ya kujichukulia sheria mikononi mwao kuacha tabia hiyo mara moja na kufuata taratibu za mkondo wa sheria ili waweze kufanya shughuli zao bila bugudha na bila kuwabugudhi wengine. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umeisha. Nina matangazo machache, Waheshimiwa Wabunge mtaona kwamba tumeshindwa kutoa nafasi kwa maswali mengi ya nyongeza kwa sababu mbili, kwanza wanaouliza maswali ya nyongeza wanatumia muda mwingi sana, pili na maswali yenyewe baadhi ya maswali ya Mawaziri ni marefu mno, nasema baadhi kwa sababu kuna jitihada kubwa sana. Majibu ni marefu mno kwa baadhi kuna jitahada kubwa sana lakini baadhi bado ni marefu. Kwa hiyo, utakuta tunamuuliza mtoa swali basi wengine hawawezi kuuliza, kwa hiyo, tujitahidi kuwa na maswali mafupi.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo matatu, kwanza kabisa baada ya kuahirisha kikao hiki saa nne na nusu Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanatakiwa kuwa na mkutano katika ukumbi wa zamani wa Bunge, Mheshimiwa Rais atakuwa na mazungumzo nao.

Waheshimiwa Wabunge, halafu pia tunaomba kutoa kwamba Kamati ya Utendaji *(Executive Committee)* ya *Amani Forum* itangaziwe kuwa leo tarehe 14/6/2006 saa 11.00 jioni katika ukumbi namba 219 uliopo gorofa ya pili katika jengo la utawala itakuwa na kikao cha muda mfupi kitachohusu mpango wa kazi za *Amani Forum* kwa kipindi hiki,

wengine wamesaini wengine hawakusaini, kwa hiyo wanachama wa *Amani Forum* wajiandae.

Lakini pamoja nasi katika ukumbi huu Mheshimiwa Waziri wa Nchi anayehusika na Bunge anaomba kwamba Waheshimiwa Wabunge wote wabaki kidogo ndani ya ukumbi baada ya mimi kumaliza kusema, kwa hiyo utabaki nikitoka.

Waheshimiwa Wabunge, lakini naomba niwatangazieni kwamba ndani ya ukumbi huu kwa mara ya kwanza tuna Waheshimiwa viongozi kutoka Wilaya ya Ilemela, wageni wa Mheshimiwa Anthony Diallo na tunafurahi kwamba hata watoto wadogo wamo, tunawakaribisha sana kwa sababu hawa wametoka mbali, kwa hiyo, ukumbi wetu unaanza kutangazwa vizuri, karibuni sana. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo, Waheshimiwa Wabunge wale ni Waheshimiwa Madiwani na viongozi wa Wilaya ya Ilemela wako 34. Waheshimiwa Wabunge, sasa taahirisha mkutano…

Kauli, mbona sikuona, Kauli ya Mawaziri, mbona *Order Paper*…

## KAULI YA MAWAZIRI

### Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2005

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2000 Bunge lilitunga sheria ya marekebisho ya iliyokuwa Sheria ya Uchaguzi ya mwaka1985. Katika marekebisho hayo kiliongezwa kifungu cha 98(2) (3). Marekebisho yote ya Sheria ya Uchaguzi yaliyofanyika siku za nyuma yaliingizwa katika Sheria ya Uchaguzi sura ya 343 ya toleo la mwaka 2002. Vifungu hivi sasa ni kifungu cha 119(2) (3), marekebisho haya yalihalalisha vitendo vya ukarimu vinavyofanywa kwa nia njema wakati wa uchaguzi kwa kuzigatia desturi za Kiafrika na ambavyo havina lengo la kuwarubuni wapiga kura kumchagua au kutokumchagua mgombea yeyote. *(Makofi)*

Mwaka 2005, Taasisi tatu zisizo za Kiserikali ambazo ni kituo cha Sheria na Haki za Binadamu yaani *Legal and Human Right Center, Lawyers and Environmental Action Team* (*LEAT* ) na *National Organization for Legal Assistant* (*NOLA),* kwa pamoja zilifungua kesi katika Mahakam Kuu ya Tanzania Masjala ya Dar es Salaam dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakidai kwamba vifungu vya sheria vilivyoingizwa kwenye sheria ya uchaguzi kwa kupitia marekebisho ya sheria ya mwaka 2000 vinakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msingi kwamba zinabagua kati ya wale wenye uwezo na wasio na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uamuzi wake uliotolewa tarehe 24 Aprili, 2006 Mahakama Kuu ya Tanzania ilikubaliana na madai ya walalamikaji na hivyo kutamka kwamba vifungu vyote vinavyohusiana na takrima yaani kifungu 119 (2)(3) na kifungu 130 (b) na ( c) ni batili kwa kuwa vinakiuka Katiba. Mahakama ilivifuta vifungu hivyo kutoka kwenye Sheria ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uamuzi huo kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za uendeshaji wa mashauri ya madai mahakamani Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ndiye mshauri mkuu wa Serikali alitoa taarifa ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo. Sababu kubwa ya kutoa taarifa hiyo ilikuwa ni kwa madhumuni ya kuzuia kinga ya muda wa kisheria wa kukataa rufaa. Aidha, lengo kuu la kutoa taarifa hiyo ya kukata rufaa ni kuiwezesha Serikali kupata fursa ya kupitia hukumu hiyo kwa madhumuni ya kujiridhisha usahihi wake kabla ya kuendelea na nia ya kukata rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imepitia hukumu kwa makini na kubaini kwamba yapo maeneo ambayo Serikali ingeweza kuhitaji kuona kwamba yanapatiwa tafsiri sahihi na mahakama ya rufaa. Hata hivyo, baada ya mashauriano na kuzingatia tamko la Mheshimiwa Rais wakati akizindua Bunge hili Tukufu ambapo aliahidi kushughulikia suala la takrima ambalo limekuwa likitolewa tafsiri mbalimbali kwa kulihusisha na rushwa. Tumekubaliana kutoendelea na rufaa hiyo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Serikali haitakata rufaa dhidi ya uamuzi huu wa mahakama, kwa sababu kufanya hivyo haitakuwa kwa manufaa ya umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkutano uliopita wa Bunge lako hili Tukufu, Serikali iliahidi kuanzisha mjadala wa Kitaifa kuhusu suala la takrima na masuala mengine pamoja na suala pana zaidi linalohusu gharama za uchaguzi. Bila shaka wote tunafahamu kwamba haiwezekani kuwepo uchaguzi wowote usiokuwa gharama. Hata tulipokuwa katika mfumo wa chama kimoja zilikuwepo gharama zilihitaji kubebwa, hata hivyo ilikuwa rahisi kulisimamia suala la gharama hizo wakati huo. Kwa mfano, wagombea waliweza wakafanya kampeni kwa pamoja wakatumia gari moja, wakawa na kikao kimoja na kama ilibidi kulala nje basi walikaa sehemu moja. Utaratibu wa kusimamia gharama hizo ulikuwa rahisi wakati huo, baada ya kuingia mfumo wa vyama vingi sasa inabidi suala hili la gharama katika uchaguzi liangaliwe upya.

Kwa kuwa Serikali ilikwishaanza mchakato wa kutafuta utaratibu utakaosimamia gharama za uchaguzi hususani wakati wa kampeni hata kabla ya uamuzi huo wa mahakama, tumeona kwamba pamoja na kwamba yapo masuala ya kisheria ambayo yangehitaji kutafsiriwa na mahakama ya rufaa si muafaka kwa sasa kukata rufaa ili mchakato huo tuliouanzisha uweze kuendelea na kukamilishwa mapema na baada ya kukamilisha kazi hiyo Wizara yangu itawasilisha Serikalini mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi yatakayozingatia pamoja na mambo mengine uamuzi wa mahakama kuhusu suala hili. Kama mapendekezo hayatakubalika na nina hakika yatakubalika, Serikali itawasilisha katika Bunge hili Muswada kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya awamu ya nne bado itazipitia sheria zote zinazolalamikiwa ili kuona namna ya kuziboresha kwa madhumuni ya kukuza demokrasia nchini na utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia kwako wananchi wavute subira kwa kuwa Serikali itaendelea kulishughulikia kikamilifu yale yote yanayoonekana kuwa kero kwao ili kuleta maendeleo ya demokrasia ya kweli nchini na utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mgombea binafsi katika uchaguzi wa Rais na Wabunge Serikali imeona kwamba kuna maeneo fulani kwenye uamuzi huo ambavyo ni vyema yawekwe mbele ya mahakama ya rufaa kutolewa uamuzi. *Notice* ya kuomba rufaa tayari imewasilishwa na kinachosubiriwa hivi sasa ni kumbukumbu za mwenendo wa kesi ili kukamilisha zoezi la kuomba rufaa. Hivyo naona haitakuwa busara kuendelea kulizungumzia suala hili mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu, kesho ndio siku ya Bajeti, asubuhi tutamsikiliza Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji halafu baadaye mchana saa kumi ndio tutakuwa na Waziri wa Fedha atakayetoa hotuba yake.

Kwa hiyo, kwa sababu hiyo naomba niahirishe kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 04:15 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi tarehe 15 Juni, 2006 saa tatu asubuhi)*